



## PRESS RELEASE

### EMBARGO

Yaliyomo ya kutolewa kwa waandishi wa habari hii na ripoti inayohusiana haipaswi kuchukuliwa au kwa muhtasari katika magazeti, matangazo au vyombo vya habari vya elektroniki kabla ya **Novemba 22, 2017, 5pm. GMT**

(Saa 12 jioni, New York, 6 jioni, Geneva; 10.30 p.m., New Delhi, 2 asubuhi, 23 Novemba 2017, Tokyo)

UNCTAD/PRESS/PR/2017/37\*

Original: English

### LDC - MAENDELEO KATIKA NCHI MASKINI ZAIDI DUNIANI YANATEGEMEA UPATIKANAJI WA NISHATI YA KISASA, INASEMA RIPOTI MPYA YA UMOJA WA MATAIFA.

Geneva, Uswisi, (22 Novemba 2017) - Kupanua upatikanaji wa vyanzo vya kutosha, kuaminika na nafuu vya nishati ya kisasa ni muhimu iwapo mataifa maskini zaidi duniani yanataka kuepuka mtego wa umaskini, inasema [Ripoti ya UNCTAD ya Nchi Maskini Zaidi Duniani ya mwaka 2017: Upatikanaji wa Nishati iletayo Mabadiliko](#).

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, iliyochapishwa leo, nchi maskini zaidi duniani (LDCs) zipo nyuma sana ya nchi nyingine zilizoendelea katika suala la kupata umeme kwa ajili ya makazi na biashara. Wakati zikiwa zimepiga hatua kubwa katika miaka ya hivi karibuni, kufikia lengo la kimataifa ya upatikanaji wa nishati kwa wote mwaka 2030 itahitaji ongezeko la asilimia 350 ya kiwango cha usambazaji umeme kwa mwaka.

"Kufikia Lengo la 7 la Maendeleo Endelevu sio tu suala tu la kutosheleza mahitaji ya nishati ya msingi ya kaya," Katibu Mkuu wa UNCTAD Mukhisa Kituyi alisema mjini Geneva, kabla ya uchapishaji wa ripoti siku ya Jumanne. "Hiyo yenyewe ina maana ya ustawi wenye thamani, lakini tunahitaji kwenda zaidi ya hapo... Ili usambazaji umeme uweze kubadilisha uchumi wa LDCs, utoaji wa nishati ya kisasa unatakiwa kuchochea ongezeko la uzalishaji na kufungua uzalishaji wa bidhaa na huduma zaidi."

Dk. Kituyi aliongeza: "Matumizi yenye manufaa ya nishati ni yale yanayobadilisha upatikanaji kuwa maendeleo ya kiuchumi, na yale yanayohakikisha kuwa uwekezaji katika miundombinu ya umeme yana manufaa ya kiuchumi. Lakini hiyo inamaanisha kuangalia zaidi ya kutosheleza mahitaji ya msingi

\* **Contacts:** UNCTAD Communications and Information Unit, +41 22 917 58 28, +41 79 502 43 11, [unctadpress@unctad.org](mailto:unctadpress@unctad.org), <http://unctad.org/press>

To receive our press material, please register at: <http://unctad.org/en/Pages/RegisterJournalist.aspx>.

<sup>1</sup>: Afghanistan, Angola, Bangladesh, Benin, Bhutan, Burkina Faso, Burundi, Cambodia, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Chad, Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Djibouti, Eritrea, Ethiopia, Gambia, Guinea, Guinea-Bissau, Haiti, Kiribati, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Lao, Lesotho, Liberia, Madagascar, Malawi, Mali, Mauritania, Msumbiji, Myanmar, Nepal, Niger, Rwanda, Sao Tome na Principe, Senegal, Sierra Leone, Visiwa vya Solomon, Somalia, Sudan Kusini, Sudan, Timor-Leste, Togo, Tuvalu, Uganda, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Vanuatu, Yemen na Zambia.

ya kaya ili kufanikisha upatikanaji wa nishati yenye kuleta mabadiliko – kutosheleza mahitaji ya wazalishaji ya nishati ya kutosha, kuaminika na nafuu."

Uhusiano huu wa pande mbili kati ya matumizi ya uzalishaji wa nishati na maendeleo ya kiuchumi, ambayo ripoti imeuita "dhana ya mageuzi ya nishati", bado ni dhaifu sana katika LDCs. Zaidi ya asilimia 40 ya biashara zinazoendeshwa katika nchi hizi zinarudishwa nyuma na upatikanaji duni, usio na uhakika na usio nafuu wa umeme. Kwa wastani, wanaumizwa kwa kukosa umeme mara 10 kwa mwezi, yanayodumu kwa takribani saa tano, na hii inawagharimu asilimia 7 ya thamani ya mauzo yao.

Wakati kwa wastani asilimia 10 ya watu katika nchi nyingine zinazoendelea wanakosa umeme, hii inabaki kuwa kadhia kwa zaidi ya asilimia 60 ya watu katika LDCs. Na nchi za LDCs kama kikundi zina karibu asilimia 8 ya uwezo wa nchi nyingine zinazoendelea wa kuzalisha umeme kwa kila mtu, na karibu asilimia 2 ya mataifa tajiri zaidi.

### **Ni wakati wa wahisani kutimiza ahadi zao za misaada**

Kufanikisha upatikanaji wa jumla wa nishati ya kisasa kwa nchi za LDCs kufikia mwaka 2030 ni gharama kubwa. Kulingana na makadirio ya awali, ripoti inaweka gharama kuwa dola za Kimarekani bilioni 12 hadi dola bilioni 40 kwa mwaka. Upatikanaji wa nishati iletayo mabadiliko bado utakuwa na gharama zaidi.

Mpaka sasa kiasi hicho kimezidi rasilimali zilizopo, ripoti hiyo inasema. Jumla rasmi ya misaada ya maendeleo kwa sekta ya nishati ni dola za Kimarekani bilioni 3 kwa mwaka, rasilimali za ndani kwa ajili ya uwekezaji wa umma ni haba katika nchi nyingi za LDCs, na nyingi pia zinakabiliwa na kikomo cha kukopa bila kuwa kwenye hatari ya mzigo wa madeni usio endelevu.

Wawekezaji binafsi huonesha shauku ndogo katika uwekezaji kwenye miundombinu ya umeme kwenye nchi za LDCs, ambao unahusisha gharama kubwa isiyoweza kufidiwa, muda mrefu wa mizunguko ya mradi na malipo ya taratibu. Nchi nyingi za LDCs huonekana kama zina mazingira magumu – ingawa upatikanaji wa huduma za kuondoa hatari hizo, kama vile bima na dhamana ya bidhaa, zinaweza kusaidia kuongeza imani kwa wawekezaji.

Serikali zinaweza kuongeza mtaji wa ziada kwa kuendeleza masoko ya deni la ndani au kutumia vyanzo mbadala vya fedha, kama vile wawekezaji wenye malengo ya kijamii, fedha ya miundombinu na, katika baadhi ya LDCs, watu wanaoishi ughaibuni.

Itakuwa vizuri zaidi, ripoti hiyo inasema, kwa wahisani wa kimataifa wakitimiza ahadi zao za muda mrefu za kutoa angalau asilimia 0.15-0.20 ya mapato yao taifa kama msaada, kama sehemu ya programu ya Istanbul ya Utekezaji kwa ajili ya Nchi Maskini Zaidi Duniani kwa Muongo wa 2011 – 2020 wa Umoja wa Mataifa. Viwango vya misaada kwa sasa kwa LDCs haukufikia lengo hilo kwa dola za Kimarekani 33 bilioni hadi dola bilioni 50 kwa mwaka.

### **Nishati mbadala ina uwezo ila itahitaji msaada**

Vyanzo vya nishati mbadala, kama vile nishati ya jua na upepo, vinaweza kuwa na matokeo ya kimapinduzi katika maeneo ya vijijini, vikihudumia asilimia 82 ya wale wasio na umeme katika LDCs, na kuwasaidia kushinda vikwazo vya kihistoria vya usambazaji wa umeme vijijini.

Lakini nishati mbadala isiyo ya maji katika nchi hizi hadi sasa imetokana zaidi na teknolojia ndogo, kama vile taa za jua na mifumo ya kipekee ya nyumbani. Wakati hawa wameleta maendeleo kiasi fulani, wamepungukiwa uwezo wa kuleta mabadiliko makubwa ya kupata umeme ambao LDCs zinahitaji ili kubadilisha uchumi wao.

Matumizi ya teknolojia mbadala yenye uwezo wa kulisha gridi na gridi ndogo ni muhimu sio tu kwa umeme wa majumbani, lakini pia kukuza biashara na viwanda, kuna haja ya kusambazwa haraka. Lakini ili kufikia lengo hili, lazima LDCs zishinde vikwazo muhimu vya kiteknolojia, kiuchumi na kitaasisi. Hii itahitaji sera za taifa na msaada wa nguvu zaidi wa kimataifa.

Licha ya uwezo usio kifani katika LDCs, nishati ya upepo na jua peke yake haiwezi kukidhi mahitaji yao. Umeme wa maji pia una mchango mkubwa, kwa sasa ukitoa nusu ya umeme unaozalishwa

katika LDCs; na mafuta ya kisukuku bado yatakuwa yanahitajika katika mambo mengi, na mabadiliko endelevu kuelekea kwenye teknolojia isiyo na kaboni nyingi kama vile gesi asilia.

Kwa sababu teknolojia za nishati, na hasa teknolojia mbadala, daima hubadilika, ni muhimu kwa LDCs kupata teknolojia inayofaa kwa hali zao maalumu na mazingira, na kwamba wanaimarisha uwezo wa sekta zao za nishati ili kunyonya teknolojia hizo.

Benki ya Teknolojia iliyoanzishwa hivi karibuni kwa ajili ya Nchi Maskini Zaidi Duniani inaweza kusaidia, lakini nchi zilizoendelea zingeweza kusaidia zaidi kwa kutekeleza wajibu wao wa kuhamisha teknolojia chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mfumo wa Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Itifaki ya Kyoto.

[Video](#)

\*\*\* \*\* \*\*\*